



Waadhini wote watakuwa na shingo ndefu zaidi kuliko watu wote siku ya Kiyama

Imepokelewa kutoka kwa Jabiri radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema:
Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu -rehema na amani ziwe juu yake- akisema:
"Waadhini wote watakuwa na shingo ndefu zaidi kuliko watu wote siku ya Kiyama".

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Muslim]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba waadhini wote ambao huwaita
watu kuja katika swala ndio watakuwa watu wenye shingo ndefu zaidi siku ya Kiyama kwa
sababu ya utukufu wa amali yao, na wingi wa kheri zao, na ukubwa wa malipo yao.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/10115>

